



Fifth EsF Assembly  
Hyderabad, India  
30 July-August 13, 2016

Montessori Education for Social Change  
Serving Humanity - Celebrating Solidarity

## 2016 EsF Assembly Daily Summary

### Saturday, 6 August 2016

---

Lynne Lawrence alifungua siku kwa nukuu ya siku toka kwa Nelson Mandela ambayo ilitolewa na mmoja wa washiriki wa mkutano wa Nne wa WWM uliofanyika Thailand. Lynne alikutana na wawakilishi toka kwa Ofisi ya Wilaya ambayo inaangalia shule 3000. Baada ya siku mbili za mazungumzo aliweza kuzungumzia mradi wa majaribio kwa shule 25 ambazo zitachukuliwa. Anne Kelly aliwasilisha mada iliyojulikana kama 'Badilisha maisha: toka huduma ya watu wenye umri mkubwa kwenda huduma ya watu wenye umri mkubwa Kimontessori'. Uwasilishaji wa Anne ulikuwa wenye nguvu na wenye hisia kwa kutupa changamoto kufikiria maisha katika mtazamo wa umri mkubwa. alitonyesha Video toka vituo mbalimbali vinavyotoa huduma ya watu wenye uri mkubwa ili kuonyesha ufanisi mkubwa wa mbinu za Kimontessori, hasa kwa mazingira ya watu wenye shida ya akili/kumbukumbu. Kwa Anne hatua ya msingi ni huduma ilikuwa ni kutafuta uwezo wa mtu. Kwa kile cha ziada tukifanyacho kwa wazee ndicho kinaiba uhuru wao. Anne alitoa mifano mbalimbali kwa undani kwa mazingira yaliyoandaliwa ambapo wajibu na kazi zenye kuleta maana zilianzishwa.

Mchana, Christine Harrison alitoa mada juu ya kujitolea, kama kazi ambayo inahitaji matayarisho, ushiriki na ushiriki wa baada ya kazi (kumweleza mwingine). Christine alitoa mfano wa kazi alizozifanya Thailand kwa kutarajia yasiyo tarajiwa. Pia alitoa changamoto na mafanikio ya watu wawili waliojitolea kufanya kazi katika mazingira ya Montessori: Cathy Swan, aliyeenda kwenye kijiji che shule yenye watu wa asili ya Australia kwa wiki mbili na Eileen aliyetumika Timor- Leste. Christine alialika watu wa tano kama sehemu ya uwasilishaji wa mada yake na kuonyesha madhara ya kiwewe. Na Lynne alijiunga na Christine katika kuigiza jinsi ya kutoa msaada.

Katika sehemu ya wazi, Solanye Cabrera alitoa mada juu ya kazi yake katika mazingira ya watu wenye lunga mbili maeneo ya Minneapolis/ St Paul. Bai Ling alizungumzia juu ya Umoja wa kujitolea Montessori nchini China na kazi ya kuwafikia watoto. Na mwisho wa siku Nagarjun Karnatkam alionyesha uwezo wake kama mwana mazingaombwe na mtu anayecheza ma akili. Vinywaji kabla ya chakula vilitolewa na wenyeji waliotupokea toka India na baada ya chalula cha jioni shamrashamra ziliendelea kwa watu kucheza muziki.